**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**SHULE YA SEKONDARI LUPALILO**

**S.L.P 51,**

**MAKETE**

**30/12/2022**

**NDUGU MZAZI/MLEZI WA ………………………………………………….**

**YAH: MAAGIZO YA UJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LUPALILO KIDATO CHA KWANZA 2023**

## 1.0.UTANGULIZI

Ninayo furaha kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2023.

Shule ya sekondari Lupalilo iko umbali wa kilometa thelathini (30) kutoka makao makuu ya wilaya ya Makete hadi shule ilipo mji mdogo wa Ikonda.Km 80 kutoka Makao makuu ya Mkoa wa Njombe, na km 3 kutoka stendi kuu ya Mabasi ya Tandala (IKONDA) hadi shuleni.

Usafiri ni wa pikipiki/ bodaboda Kutoka stendi ya mabasi Tandala au Hosipitali ya Ikonda hadi shuleni kwa Tshs 2000/= tu.

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe ----------------------- hivyo mzazi unatakiwa kumleta mwanao shuleni tayari kwa kuanza masomo , mwisho wa kuripoti ni tarehe -------------------- ndani ya siku saba za masomo.

## 2.0. SARE YA SHULE

### (a) KWA WAVULANA

1. Suluwali jozi 2 ,rangi nyeusi chini ziwe na upana wa sm16 au zaidi
2. Shati mbili nyeupe za mikono mirefu
3. Sweta jozi 2, za rangi ya blue zenye kola ya (v)
4. Kiatu cheusi cha kamba kisicho na mchongoko mbele na kisiwe na kisigino kirefu
5. T- sheti moja yenye nembo ya shule rangi darkblue itapatikana shuleni kwa tshs 12000/=
6. Tack-suti nyeusi yenye ufito mweusi

### (b) **KWA WASICHANA**

1. Suluali jozi 1 na sketi 1, rangi kijani CCM - ISTIM namba moja (zisiwekwe lastiki)na sketi iwe ndefu cm 15 kutoka kwenye kisigino. Zingatia urefu wa sketi
2. shati jeupe mikono mirefu moja na Blauzi nyeupe za mikono mirefu jozi 1, (nusukanzu)

3. Sweta jozi 2, rangi ya blue zenye kola ya (V)
4. Viatu vyeusi vya kamba visivyo na mchongoko mbele na visiwe na kisigino kirefu
5. T- sheti moja yenye nembo ya shule rangi darkblue itapatikana shuleni kwa tshs 12000/=
6. Track suti nyeusi yenye ufito mweupe

2.1 **SARE ZA MICHEZO**

- **KWA WASICHANA**

1. Bukta na flana rangi nyekundu (jozi moja)
2.Raba za michezo rangi nyeusi (jozi moja)
3.Soksi ndefu nyeupe jozi 2 za michezo

- **KWA WAVULANA**

1. Bukta na flana rangi nyeupe (jozi moja)
2. Viatu nyeusi vya michezo vyenye njumu chini (jozi moja)
3. Soksi ndefu nyeusi jozi 1, za michezo

3.0. **VIFAA VYA DARASANI / TAALUMA**

1. Daftari 12 counter book kwaya three (3) au zaidi

` 2. Biki za kuandikia 12, penseli 5 za kucholea, rula ndefu 2, mkebe 1,

4. Dikishonari ya kingereza kwa Kiswahili moja
5. Rimu 1 A4 ya karatasi kwa ajili ya mitihani ya wiki na mwezi
6. Jalada moja la tshs 1500, kwa ajili ya kutunza taarifa zake binafsi
7. Mzazi unaweza kununua vitabu mbalimbali vya sekondari kwa ajili ya mwanao kujisomea

4.0. **HUDUMA YA HOSTELI**

1. Shule yetu ni shule ya kutwa kwa kidato cha kwanza hadi cha nne, hivyo shule ina hosteli na utaratibu wa kutoa huduma ya Hosteli kwa wanafunzi wa kike na wakiume wachache watokao mbali na shule na wenye uhitaji na uwezo wa kulipa mchango wa chakula na wapishi. Pia kwa wanafunzi wa kutwa nje ya hosteli shule kwa kushirikiana na kamati ya chakula ya wazazi inautaratibu wa kutoa uji na chakula cha mchana kwa wanafunzi wote ambao wazazi wao wameweza kuwachangia fedha ya chakula .
Gharama kwa huduma hiyo ni kama ifuatavyo.

4.1. **KWA WANAFUNZI WA HOSTELI** (WATAKAO KUWA TAYARI KUKAA HOSTELI TU)
1. Chakula,wapishi na matroni Tshs 375,000/= kwa mwaka pia gharama hiyo inaweza kulipwa kwa awamu mbili (muhula wa kwanza Tshs 187,500/= na muhula wa pili tshs 187,500/=)

**MUHIMU;**Fedha zote zilipwe kwenye akaunti namba **0133669201200** yevye jina la **wazazi hostel tandala CRDB BENKI** Pia naomba ifahamike kukaa hosteli inategemea sana mchango wako wa chakula hivyo bila kulipa hautaruhusiwa kumleta mwanao hosteli.MZAZI HAKIKISHA UNAKUJA NA HATI YA MALIPO SHULENI ULIYOLIPIA BENK

4.2.**KWA WAVULANA NA WASICHANA WA KUTWA**.(KWA AJILI YA UJI NA CHAKULA CHA MCHANA TU)

1. Chakula na posho za wapishi Tshs 187,500/= kwa mwaka, unaweza kulipa awamu mbili Tshs 93,750/= kwa muhula

2. Vyombo vya chakula (sahani ,bakuli , kikombe, kijiko na uma)

4.3. **VIFAA MUHIMU KWA WANAFUNZI WA HOSTELI**

i).Godoro 2.5 x 6 (moja)
ii).Tranka (sanduku la kuhifadhia vifaa vyake akiwa hosteli)
iii). Shuka rangi light blue na mto mmoja
iv). Mahitaji mengine ndala za kuogea jozi 1, taulo 1, sabuni ya kuogea 3, sabuni za kufulia miraba 2, mafuta ya kupaka, dawa ya meno ,miswaki 2, yebo jozi 1,na kandambili jozi 1
v). Pia utampatia mwanao fedha za matumizi yake binafsi
vi). Ndoo moja ya lita 10 kwa ajili ya matumizi yake binafsi
vii). Vyombo vya chakula(bakuli , sahani , kikombe, kijiko na uma

**5.0. MAAGIZO YA VIFAA VYA KAZI NA USAFI KWA WAVULANA NA WASICHANA**

1. Jembe moja jipya lenye mpini
2. Fagio moja la chelewa
3. Ndoo moja ya lita 10

**6.0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya waziri Mkuu TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa/pangiwa na viongozi au walimu.
e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii.
f. Kutunza usafi wa mwili mavazi na mazingira ya shule
g. Kuvaa sare ya shule wakati wote uwapo shuleni au upatapo ruhusa ya kwenda nje ya mipaka ya shule
h. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote uwapo shuleni
i. Kutunza mali za umma kwa uzalendo mkubwa wakati wote wa uwanafunzi wako

## 7.0. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE MWANAFUNZI

a. Wizi
b. Uasherati
c. Ubakaji
d. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi,kubeli, na kadhalika
e. Kupiga au kupigana
f. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g. Kudharau bendera ya Taifa
h. Kuwa mjamzito kupata mimba
i. Kuoa au kuolewa
j. Kutoa mimba
k. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
l. Kukataa adhabu kwa makusudi
m. Kuwa na simu ya mkononi au line ya simu au kamela
n. Kutoka nje ya mipaka ya shule bila ya ruhusa
o. Kutoandika darasani, kutokuwa na madaftari ya masomo kwa ngazi yoyote kwa madarasa uliyoyapitia hapa shuleni
p. Kutoingia darasani zaidi ya siku tisini/ miezi mitatu
q. Kwenda kwenye nyumba za walimu bila ruhusa
r. Kutofuata ratiba za shule
s. Kumiliki na Kutumia simu tofauti na simu ya shule
t. Pia kosa/ makosa mengine yoyote yatakayoenda na muunganiko wa makosa yaliyoandikwa hapa.

**MINISTRY OF EDUCATION SCIENCE, TECHNOLOGY & VOCATIONAL TRAINING**
**REQUEST FOR MEDICAL EAMINATION**

**LUPALILO SECONDARY SCHOOL**
**P.O.BOX 51,**
**MAKETE**
**DATE …………………**

**TO THE MEDICAL OFFICER**
**……………………………………….**
**……………………………………….**

**PART. A**

**Mr/Mrs/ Miss ……………………………………………………….**

Please examine the above named pupil as to her physical and mental fitness for a full time student in this school. The examination should include the following categories.

1. Hemoglobin
2. P.v bleeding
3. Eye sight
4. Blood pressure
5. Urine and sugar
6. Stool for routine examination
7. Asthma
8. Skin diseases
9. Leprosy
10. Epilepsy
11. Any deformity
12. Pulmonary tuberculosis
13. Neurosis
14. Venereal diseases
15. Other serious diseases
16. Pregnancy

Thank you

**……………………**
**LUNANILO KILATU**
**DEPUTY HEAD OF SCHOOL**

**PART. B**

(To complete by government medical officer)

1. I have examined the above named pupil and consider that she is physical and mental fit/ until for full time schooling
2. Other comments
   ……………………………………………………………………………………………………
   …………………………………………………………………………………………………….
   Name ……………………………………………. Signature
   ……………………………………………………….
   Official stamp
   …………………………………………………Designation…………………………

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**

**SHULE YA SEKONDARI LUPALILO**

**FOMU YA MAPATANO/ KUKUBALI NAFASI YA MASOMO YA KUSOMA KATIKA SHULE HII KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2023**

Kabla ya kusaini soma kwa makini maagizo yote. Shule haitapenda usumbufu wa aina yoyote ile usio na msingi.

JINA LA MWANAFUNZI ……………………………………………………………………………………

ANWANI ………………………………………………………………………………………………..

MIMI ……………………………………………………………………………………………………

Nimekubali /sikubali kujiunga na jumuiya ya shule ya sekondari lupalilo Nimesoma maagizo ya shule kwa makini na kuyaelewa , nahidi kuwa mtiifu na kuzingatia sheria , taratibu za shule kinyume chake hatua kali za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu ikiwa pamoja na kufukuzwa shule.

Naadi kusoma kwa bidii masomo yangu na kufaulu mitihani itakayotolewa na shule, wilaya mkoa na taifa.

Sahihi ya mwanafunzi ……………………………………Tarehe ……………………………………………

Mimi Mzazi/ mlezi wa mwanafunzi ………………………………………..wa kidato cha……………mwaka………..

Nimesoma kwa makini maagizo ya shule yaliyotolewa kwa mtoto wangu nimekubali / sijakubali …………………….mwanangu achukue nafasi hiyo.

Nahidi kuwa nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumkuza na kumlea mwanafunzi huyu kielimu na kitabia, pia nahidi kumlipia fedha ya chakula , fedha za matibabu na michango mingine mbalimbali tutakayokubalia katika vikao vyetu vya wazazi na shule kwa wakati muafaka , kinyume na hapo nichukuliwe hatua za kisheria.

Sahihi ya mzazi / mlezi ………………………………………………..

NB.Fomu hii itawekwa kwenye jalada la mwanafunzi kwa kumbukumbu zaidi

**…………………………**

**LUNANILO KILATU**

**KAIMU MKUU WA SHULE**)

**0763228809**